



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO
MAMLAKA YA UDHIBITI WA UNUNUZI WA UMMA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. GA.128/192/01/'F"/38

6 Julai, 2023

Maafisa Masuuli;

Taasisi Nunuzi Nchini;

TANZANIA BARA.

**YAH: MATUMIZI YA MFUMO MPYA WA UNUNUZI KWA NJIA YA MTANDAO (NeST)
NA UWASILISHAJI WA MPANGO WA UNUNUZI WA MWAKA 2023/24**

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) inapenda kuwajulisha kuwa Serikali imejenga Mfumo mpya wa Ununuzi kwa Njia ya Kielektroni (NeST) ambapo Taasisi kadhaa zimeanza kuutumia kuanzia tarehe 1 Julai 2023. Kutokana na kukamilika kwa Moduli za **e-registration** na **e-tendering** za Mfumo huo na kwa kuwa Mkataba wa matumizi ya Mfumo wa TANePS unaisha Mwezi Disemba 31, 2023, Serikali imeelekeza Taasisi Nunuzi zote zianze kutumia Mfumo huu katika ununuzi wote unaotumia fedha za umma.
3. Kwa kuzingatia maelezo yaliyotolewa hapo juu, PPRA inatoa maelekezo yafuatayo kwa Taasisi Nunuzi zote, juu ya matumizi ya Mifumo ya NeST na TANePS:

(a) TAASISI NUNUZI AMBAZO ZIMEPATIWA MAFUNZO YA NEST

Taasisi Nunuzi zote ambazo zimeshapatiwa Mafunzo ya NeST hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023, zinatakiwa kutumia Mfumo huu badala ya TANePS. Taasisi hizi zinatakiwa kuandaa Mpango wa Mwaka wa Ununuzi (APP) kupitia kwenye NeST na kuhakikisha kuwa zabuni zao zinachakatwa kwenye Mfumo mpya kwa manunuzi yanayofanyika kuanzia Mwaka huu wa fedha 2023/2024.

(b) TAASISI NUNUZI AMBAZO HAZIJAPATIWA MAFUNZO YA NEST

Taasisi Nunuzi zote ambazo hazijapatiwa Mafunzo ya NeST hadi kufikia tarehe 30 Juni 2023 zinatakiwa kuendelea na matumizi ya TANePS hadi tarehe 30 Septemba



2023, ambapo matumizi ya mfumo huu yatasitishwa. Taasisi hizi zinatakwa kuendelea kutumia utaratibu wa awali wa kuwasilisha APP kwa ajili ya kuidhinishwa kwenye TANEPS na kuhakikisha manunuzi yanayofanyika kwenye mfumo huu ni yale yanayoweza kukamilika kabla ya tarehe 30 Septemba 2023. Michakato yote ambayo haitaweza kukamilika kufikia tarehe 30 Septemba 2023 inatakiwa ifanyike kwenye NeST.

Vile vile, Taasisi hizi zinatakiwa kuhakikisha zinapeleka Watumishi wao kwenye mafunzo ya matumizi ya NeST na kuhakikisha wanapata mafunzo ya mfumo huu kabla ya tarehe 30 Septemba 2023. Kuanzia tarehe 1 Oktoba 2023, michakato yote ya ununuzi wa umma itafanywa kupitia Mfumo wa NeST.

(c) MANUNUZI YA VIFAA NA HUDUMA MTAMBUKA KWENYE TANEPS (CUIS)

Taasisi Nunuzi zote zinajulishwa kuwa zitaendelea kutumia mfumo wa TANEPS kwa Ununuzi wa Vifaa na Huduma Mtambuka (Common Use Items-CUIS) hadi tarehe 30 Septemba 2023. Kuanzia tarehe 1 Oktoba 2023, Taasisi Nunuzi zote zitakuwa zikitumia mfumo wa NeST kwenye ununuzi wa Vifaa na Huduma Mtambuka.

4. Nawatakia utekelezaji mwema.



Eliakim C. Maswi
AFISA MTENDAJI MKUU